WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 61 | Dec 1 - 30 2024




# HISTORIA NYINGINE YAANDIKWA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE (JNHPP)

WIZARA YA NISHATI +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Prudence Constantine

**WAANDISHI**

Theresa Mhagama
Hafsa Omary
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika

**WAPIGA PICHA**

Amanzi Kimonjo
Henry Kilasila
Mustafa Shahame
Isaya Mwakajana

**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga


© NISHATI 2024

# HISTORIA NYINGINE YAANDIKWA MRADI WA UMEME WA JULIUS NYERERE (JNHPP)

- Dkt.Biteko azindua mradi wa usafirishaji umeme (kV 400) Chalinze-Dodoma na upanuzi wa vituo vya umeme Chalinze na Zuzu
- Kuwezesha umeme kutoka JNHPP kufika Kanda mbalimbali za Tanzania, Migodi ,Viwanda, Kusini na Mashariki mwa Afrika
- Asema Tanzania inaongoza Afrika kwa Usambazaji wa umeme kwa wananchi
- Apaza sauti kwa wahujumu wa miundiombinu ya umeme; Ataka hatua kali zichukuliwe



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko (Wa tano kutoka kushoto), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe.Innocent Bashungwa (wa kwanza kulia) Naibu Waziri wa Nishati Mhe Judith Kapinga ( Wanne kutoka kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule (Wa nne kutoka kulia), Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakari Kunenge (wa tatu kutoka kulia), Katbu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba (wa tatu kutoka kushoto) na Mkuu Mkoa wa Morogoro Adam Malima ( wa pili kutoka kulia) wakifunua kitambaa katika jiwe la msingi la Ujenzi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Chalinze hadi Dodoma na upanuzi wa vituo vya umeme vya Zuzu-Dodoma na Chalinze Pwani tarehe 11 Desemba 2024, Jijini Dodoma.

Tanzania imeandika historia nyingine katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya umeme baada ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe.Dkt.Doto Biteko kuzindua utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya kilovoti 400 Chalinze-Pwani na Zuzu-Dodoma.

Mradu huo wa umeme uliozinduliwa utawezesha umeme wote unaozalishwa katika mradi wa kuzalisha umeme wa JNHPP kufika katika maeneo yote ya mikoa iliyopo Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati na Kanda ya Magharibi, Migodi, Viwanda na kuimarisha biashara ya umeme Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Dkt. Biteko amesema kuteklezwa kwa mradi huo kunatokana na Rais, Dkt.Samia Suluhu Hassan kuendelea kutoa fedha za kutekeleza miradi mbalimbali pamoja na miongozo yake ya namna bora ya kutekeleza miradi ili kuhakikisha nchi inakuwa na umeme wa uhakika kwa lengo la kukidhi mahitaji ambayo yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku kutokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Amesema kuwa kutokana na jitihada hizo zinazofanywa na Rais Samia katika kuendeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme imepelekea Tanzania kuwa kinara barani Afrika katika usambazaji wa umeme kwa wananchi na hii ni kutokana na takwimu zilizotolewa na Benki ya Dunia

Ameeleza kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na jitihada za kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme nchini ambazo zimewezesha kuongeza uwezo wa mitambo ya kufua



Muonekano wa Kituo cha umeme cha Zuzu Dodoma ambacho kitapanuliwa chini ya mradi wa Upanuzi wa vituo vya umeme vya Zuzu-Dodoma na Chalinze-Pwani

umeme iliyopo nchini hadi kufikia Megawati 3,169.26 ambapo mahitaji ya juu ya umeme nchini kwa sasa yamefikia Megawati 1,888.72 ambapo mahitaji hayo hayajawahi kufikiwa kutoka nchi ipate Uhuru na hii ikimaanisha kuwa uchumi unazidi kukua kutokana na kuongezeka kwa shughuli za maedeleo. "Kuimarika kwa uzalishaji wa umeme nchini kumechangiwa na kuanza uzalishaji katika Mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 2,115 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 99.6 na jumla ya Megawati 1,175 za umeme zinazalishwa na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa. "Amesema Dkt.Biteko

Katika Hafla hiyo, Dkt.Biteko amekemea vikali wahujumu wa miundombinu ya umeme ambao amesema kuwa wanarudisha nyuma uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali katika kuwafikishia wananchi nishati ya uhakika na kuagiza Vyombo vya Ulinzi na Usalama kuchukua hatua kali kwa wahujumu hao ambao oia wamekuwa wakikosesha wananchi umeme pale miyndombinu inapoharibiwa.

Kuhusu Wakandarasi wa mradi huo, Kampuni ya TBEA kutoka China, amewataka wahakikishe mradi unakamilika kwa wakati ili wananchi wapate manufaa yaliyokusudiwa ikiwa pia ni maelekezo ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Dkt.Biteko ametumia hafla hiyo kuwakumbusha viongozi na wananchi kuhusu jitihada za Serikali katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kutimiza lengo la Serikali la asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Katika muendelezo wa jitihada hizo, amesema Serikali imetoa ruzuku kwa mitungi ya gesi zaidi ya 400,000 itakayouzwa kwa nusu gharama ya bei ya soko ambapo mitungi hiyo inasambazwa katika Mikoa yote Tanzania Bara.

Ametoa wito kwa Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia kwa kutumia majiko ya gesi na teknolojia mbalimbali kulingana na mazingira ikiwemo nishati ya umeme kwani nishati hizi ni miongoni mwa nishati safi, salama na ya gharama nafuu ikilinganishwa na matumizi ya kuni na mkaa.

Vilevile ametoa wito kwa wadau mbalimbali na wafanyabiashara nchini kuhakikisha majiko yanayotumia nishati fanisi ya umeme yanapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu ili wananchi wengi katika maeneo mbalimbali wakiwemo wa vijijini waweze kutumia umeme kwa ajili ya kupikia.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Innocent Bashungwa ameipongeza Wizara ya Nishati na TANESCO kwa uzinduzi wa mradi huo wa usafirishaji umeme na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya zuzu Dodoma na Chalinze na kueleza kuwa utekelezaji wa mradi huo unaakisi dhamira ya Rais Dkt. Samia ya kutaka watanzania wapate nishati ya uhakika.

Bashungwa amesema kuwa Serikali inatoa fedha nyingi ili kutekeleza miundombinu ya umeme hivyo Wizara yake itahakikisha miundombinu hiyo inalindwa kwa wivu mkubwa na kuwashughulikia wahalifu wa moundombinu hiyo,

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga amempongeza Rais, Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanyika katika Sekta ya Nishati na pia amempongeza Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt.Doto Biteko kwa kusimamia Sekta kwa weledi, ufanisi, uzalendo na uchapakazi wa hali ya juu.

Amesema mradi uliozinduliwa leo ni muhimu kwani Tanzania inategemewa kuimarisha hali ya umeme kwa nchi za Mashariki mwa Afrika kupitia miradi ya uzalishaji na usafirishaji umeme ambayo inaendelea kufanyika.

Amesema moja ya masuala yaliyokuwa yakitiwa mkazo katika Mkutano uliohusu biashara ya kuuziana umeme na kununua umeme kwa nchi Wanchama Mashariki mwa Afrika (EAPP) ni uunganishaji umeme kati ya Tanzania na Kenya ambapo leo laini hiyo ya umeme ya kV 400 imewashwa Rais na pongezi zimetolewa kwa Rais Samia na Dkt. Bitekp.kwa kuteleleza mradi huo.

Kwa upande wake, Katibu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema sasa nchi inazalisha zaidi ya megawati 3000 za umeme na hii inaifanya Tanzania kuwa nchi inayozalisha umeme mwingi kuliko nchi zote za Afrika Mashariki na hivyo kutoa fursa kwa Tanzania kufanya biashara ya umeme na nchi nyingine za Afrika iikwemo Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya.

Amesema mradi huu utaenda katika kanda mbalimbali ikiwemo mikoa ya Kaskazini na kuingia hadi nchini Kenya.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga alisema mradi wa kusafirisha umeme kutoka Chalinze hadi Dodoma umegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme katika msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma yenye urefu wa kilomita 345 na upanuzi wa vituo vya kupokea na kupoza Umeme vya Chalinze (400/220/132kV) mkoani Pwani na Zuzu (400/220/33kV) Mkoani Dodoma.

Alisema malengo ya mradi huo ni kuwezesha usafirishaji wa umeme wote (2,115MW) utakaozalishwa katika Bwawa la JNHPP na kuufikisha kwenye maeneo yote ya mahitaji ya umeme, hatua itakayosaidia kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme kwenye Gridi ya Taifa na kuongeza uwezo wa kusafirisha umeme kwenda mikoa yenye viwanda na migodi ya uchimbaji madini ya Kaskazini Magharibi, Kaskazini Mashariki, Kanda ya Kati na Kusini mwa Tanzania.

Alieleza kuwa, lengo lingine la mradi ni kuwezesha zoezi la uunganishaji umeme kwa pamoja katika mifumo ya Mashariki mwa Afrika (Eastern Africa Power Pool - EAPP) na Kusini mwa Afrika (Southern Africa Power Pool - SAPP) na hivyo kuwezesha kufanyika kwa biashara ya nishati ya umeme kikanda (Regional Power Trading).

Aliongeza kuwa, Mradi husika unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 kwa jumla ya gharama ya Shilingi 513 Bilioni ambapo Mkandarasi Kampuni ya TBEA kutoka China ameshalipwa malipo ya awali ya kiasi cha Shilingi bilioni 107.93 ambayo ni asilimia 20 ya gharama za mradi.

Alieleza kuwa katika mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme, kazi mbalimbali zimeanza na mradi utakamilika mwaka 2026 mwezi Septemba huku mradi wa upanuzi wa vituo vya kupoza umeme kazi pia zinaendelea na mradi utakamilika Septemba 2026.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge amesema mradi huo ni uthibitisho wa kazi kubwa na nzuri za Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwamba umeme huo utafaidisja Tanzania na nchi nyingine za Afrika na ni sehemu pia ya uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia kwani wananchi watatumia umeme huo kupikia.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima amesema wananchi mkoani Morogoro wanatambua kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia katika kuendeleza miradi ya umeme ikiwemo kukamilisha miradi ya miaka mingi ukiwemo wa kuunganisha umeme kati ya Tanzania na Kenya.

Mwakilishi wa Wadau wa Maendeleo katika hafla hiyo, Wendy Hughes ambaye ni Mkurugenzi wa Benki ya Dunia Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kujikita katika kuiimarisha gridi ya taifa ya umeme ambayo ni muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii pamoja na kutoa uhakika wa usalama wa nishati.

Amesema kuwapo kwa mifumo imara ya usafirishaji umeme itafanya wananchi kufikishiwa umeme wa uhakika katika maeneo mbalimbali ya nchi na pia ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa kufikisha umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo 2030.

Ameahidi kuwa Wadau wa Maendeleo wataendelea kutoa ushirikiano kwa Tanzania ili kukamilisha mipango mbalimbali ya maendeleo ambayo nchi imejiwekea.

# SUALA LA MATUMIZI BORA YA NISHATI LIWE KWENYE MIPANGO YETU YA SERIKALI – DKT.BITEKO

- Nia ni kuhakikisha Bara la Afrika linatumia nishati kwa ufanisi na kupunguza upotevu wa umeme
- Afungua Mkutano wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati (REEC 2024)
- Azindua Mkakati wa kwanza wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati
- UNDP, WB na EU zatoa pongezi, zaahidi ushirikiano




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko (katikati), Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Geofrey Pinda ( wa nne kushoto) na Bw. Marc Stalmans ( wa tatu Kulia) kutoka Umoja wa Ulaya( EU) wakiwa wameshika Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati (2024-2034) mara baada ya kuzinduliwa na Dkt. Biteko wakati wa Mkutano wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati uliofanyika Arusha tarehe 4 Desemba, 2024.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa suala la matumizi Bora ya Nishati linapaswa kuwepo kwenye mipango ya Serikali katika nchi za Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ili kuwezesha nchi hizo kutumia umeme kwa ufanisi na hivyo kupunguza upotevu wa umeme.

Dkt. Biteko amesema hayo tarehe 04 Desemba 2024 jijini Arusha wakati akifungua Mkutano wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati (REEC 2024) ulioandaliwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Ubalozi wa Ireland ukishirikisha Viongozi na Wadau mbalimbali wa Matumizi Bora ya Nishati kutoka EAC na SADC.

Amesema pamoja na nchi mbalimbali barani Afrika kuzalisha umeme na kusafirisha kwa ajili ya matumizi lakini bado kuna chagamoto za kuhakikisha kuwa umeme huo unaozalishwa na kusafirishwa unatumika kwa ufanisi.

“ Kwa mfano kuna sababu gani ya mtu hayumo ndani ya nyumba lakini vifaa vyote vya umeme kama vile luninga, kiyoyozi, televisheni, radio na taa wakati wote vinafanya kazi, vitendo kama hivi vya kutumia umeme bila ufanisi vinaongeza mzigo kwenye uzalishaji wa umeme, umeme ambao kiasi kwa kiasi Fulani ungeweza kutumika kwa mahitaji mengine.” Amesema Dkt. Biteko

Ameeleza kuwa, takwimu za Taasisi ya Kimataifa ya Nishati (IEA) zinaonesha kuwa ufanisi wa nishati duniani umeimarika kwa asilimia 1.1 tu mwaka 2023 ikiwa ni chini ya lengo kwani kwa sasa ufanisi wa nishati unatakiwa kukua kutoka asilimia 2 hadi 4



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe, Dkt. Doto Biteko akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati uliofanyika Arusha tarehe 4 na Desemba, 2024.

hivyo ili kufikia lengo hilo nchi za Afrika zinahitaji kushirikiana katika kutatua changamoto zinazopelekea kutokuwa na matumizi bora ya nishati.

Amesema Mkutano wa REEC 2024 uwe ni sehemu ya kuweka msisitizo kuwa matumizi bora ya nishati si suala la hiari bali ni la lazima na msingi katika upatikanaji wa nishati ya uhakika, kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa na kuwa na ukuaji wa uchumi ambao ni endelevu.

"Uwepo wa Viongozi, Wataalam na wadau wa maendeleo kutoka nchi mbalimbali za Afrika utafanya mkutano wa REEC 2024 kuwa wa mafanikio kwani utahusisha pia kubadilisha uzoefu na utaalam katika matumizi Bora ya Nishati na utaiwezesha Tanzania na Bara zima la Afrika kufikia suluhisho la upatikanaji wa nishati safi." Amesema Dkt.Biteko

Dkt.Biteko ametilia mkazo uwepo wa teknolojia za kupikia zenye ufanisi wa nishati ili kupunguza gharama za nishati majumbani, kuwa na hewa safi ndani ya nyumba, na kulinda misitu dhidi ya matumizi ya kuni kupita kiasi.

Aidha ameishukuru EU, UNDP na Ubalozi wa Ireland kwa kuunga mkono Serikali katika uandaji wa Mkutano huo wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati pamoja na Benki za Kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) zinazounga mkono mikakati mbalimbali ya kuendeleza Sekta ya Nishati nchini na kutoa wito kwa wadau hao wa maendeleo kuendelea kutoa mchango wao kwenye ufanisi wa matumizi ya nishati nchini bila kusahau nishati safi ya kupikia.

Katika Hafla hiyo ya Ufunguzi wa Mkutano wa REEC 2024, Dkt. Biteko amezindua Mkakati wa kwanza wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati (2024-2034) ambao pamoja na masuala mengine unalenga kuhamasisha watanzania kutumia nishati kwa ufanisi ili kupunguza gharama za matumizi, kupunguza upotevu wa umeme na kutunza mazingira.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda amesema REEC 2024 unahamasisha fursa za ushirikiano, kubadilishana uzoefu na kuweka miongozo wa matumizi bora ya nishati katika nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Amesema siku mbili za mkutano huo zitaleta matokeo mbalimbali ikiwemo kuongeza uelewa kuhusu matumizi bora ya nishati, kutatua changamoto zinazojitokea katika utekelezaji wa mikakati ya matumizi bora ya nishati na kuwa na ushirikishaji wa Sekta binafsi katika matumizi bora ya nishati.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alisema mkutano wa REEC 2024 ni mkutano unaoendana na Sera ya Nishati ya Tanzania ya mwaka 2015 inayotambua kuwa kama taifa linahitaji nishati ya kutosha lakini inayotumiwa uangalifu, umakini na ubora ili kuhakikisha nchi haizalishi nishati isiyoihitaji na haingii gharama ambazo isingeziingia endapo ingetumia nishati kwa ufanisi.

Amesema kwa upande wa Tanzania, ili kuwa na matumzi Bora ya Nishati, Serikali ya Tanzania kwa kushirikina na Wadau wa Maendeleo inatekelza mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati utakaowezesha watanzania kutumia nishati kwa ubora na kwa uangalifu na hii ikienda sambamba na kusimamia aina ya vifaa vya umeme vinavyoingia nchini ili kuingiza vifaa vyenye ufanisi na ubora unaotakiwa.

Naibu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Amon Manyama amesema UNDP inajivunia kufanya kazi na serikali ya Tanzania katika utekelezaji wa Mradi wa Matumizi Bora ya Nishati.

Amesema Mkutano wa REEC 2024 ni muhimu katika kuhamasisha na kuchagiza matumizi sahihi ya nishati kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Kusini mwa Afrika.

Aidha, EU na WB zimeipongeza Tanzania kwa utekelezaji wa miradi ya Nishati ikiwemo mradi huo wa Matumizi Bora ya Nishati na kuahidi kuendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania kwenye miradi ya maendeleo endelevu itakayoinua uchumi wa Watanzania huku ikilinda mazingira.

# KAPINGA ATUMIA KONGAMNO LA BIASHARA NA UWEKEZAJI SAUDI ARABIA KUNADI FURSA ZA UWEKEZAJI NCHINI

- Waziri Kapinga afanya mazungumzo na Naibu Waziri wa Nishati Saudi Arabia
- Wajadili ushirikiano katika Mafuta, Gesi Asilia, Nishati Jadidifu na Nishati Safi ya Kupikia
- Saudi Arabia yaeleza kutambua juhudi za Tanzania kuimarisha Sekta ya Nishati



Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga (kushoto) na Naibu Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia,Mhandisi Mohammed Albrahim (kulia) wakizungumza kuhusu ushirikiano wa Tanzania na Saudi Arabia katika Sekta ya Nishati, wakati wa Mhe. Kapinga alipohudhuria Kongamano la Wafanyabiara na Wawekezaji lililofanyika katika tarehe 18 na 19, Desemba 2024, mjini Riyadh, Saudi Arabia.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema Tanzania itaendelea kushirikiana na Saudi Arabia katika kuimarisha Sekta ya Nishati hususan katika Mafuta na Gesi, Nishati Safi ya Kupikia na Nishati Jadidifu.

Mhe. Kapinga amesema hayo wakati alipokutana na Naibu Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Mhandisi Mohammed Albrahim katika Mji wa Riyadh tarehe 19 Desemba,2024 nchini Saudi Arabia.

Amesema kuwa, Tanzania imekuwa ikishirikiana na nchi hiyo kwa muda mrefu katika Biashara ya Mafuta na Maeneo Mengine ya Maendeleo hivyo mahusiano hayo yanaendelea kuimarika zaidi kwa kuwa mahitaji ya nishati yanazidi kuongezeka na uwekezaji zaidi unahitajika katika kuendeleza Sekta ya Nishati ikiwemo Mafuta na Gesi Asilia, Nishati Jadidifu na Nishati Safi ya Kupikia.

"Mahusiano ya Tanzania na Saudi Arabia katika Sekta ya Nishati ni ya muda mrefu, nchi hizi mbili zimekuwa na lengo la kuboresha ushirikiano wao katika kuendeleza sekta ya nishati." Amesema Kapinga

Aidha, ameeleza kuwa Tanzania kama nchi inayoendelea inahitaji kuimarisha zaidi miundombinu yake ya nishati katika maendeleo hivyo imekuwa ikishirikiana na nchi zenye uzoefu mkubwa katika sekta hizo ili kupata matokeo chanya kwa kuwa nishati ni msingi mkuu wa maendeleo.

Amesema Saudi Arabia imekuwa ikijulikana kwa uwezo wake mkubwa katika uzalishaji wa mafuta na gesi, na imekuwa ikiwekeza katika maeneo mbalimbali ya Dunia, ikiwemo Afrika Mashariki, ambapo kwa upande wa Tanzania yenye rasilimali za Gesi Asilia na viashiria vya uwepo wa Mafuta inapata uzoefu, ujuzi na teknolojia kutoka Saudi Arabia katika kuchimba, kusafisha na kusafirisha mafuta na gesi pamoja na kuimarisha miundombinu ya rasilimali hizo.

Vile vile, Mhe. Kapinga amesema kuwa kuimarika kwa Sekta ya Nishati nchini kutaiweza nchi kuweza kusambaza Umeme



Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga(kushoto) na Naibu Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Mhandisi Mohammed Albrahim(kulia) wakiwa katika picha ya Pamoja na ujumbe kutoka Tanzania na wa Saudi Arabia walipokutana baada ya kumaliza mazungumzo yao kuhusu ushirikiano wa Tanzania na Saudi Arabia katika sekta ya Nishati, wakati wa Kongamano la Wafanyabiara na Wawekezaji lililofanyika, tarehe 18 na 19, Desemba 2024, mjini Riyadh, Saudi Arabia.



Maafisa kutoka Wizara ya Nishati na Ofisi za Ubalozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia wakiwa katika kikao kati ya Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga na Naibu Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, wakizungumzia kuhusu ushirikiano wa Tanzania na Saudi Arabia katika Sekta ya Nishati, wakati wa Mhe. Kapinga alipohudhuria Kongamano la Wafanyabiara na Wawekezaji lililofanyika tarehe 18 na 19, Desemba 2024, mjini Riyadh Saudi Arabia.Kutoka kulia ni Kamishna Msaidizi wa Petroli, Mhandisi. Joyce Kisamo, Mkurugenzi Msaidizi wa Sera,Utafiti na Ubunifu, Oscar Kashaigiri na Msaidizi wa Naibu Waziri wa Nishati, Bi. Loyce Lubonera(kushoto).

utakaozalishwa nchini kwa nchi jirani ambazo zimeonyesha nia ya kuhitaji Nishati.

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati wa Saudi Arabia, Mhandisi Mohammed Albrahim amesema kuwa nchi yake inajipanga kuwekeza zaidi katika ujenzi wa Miundombinu ya barabara, utunzaji wa mazingira na kuwekeza zaidi katika Sekta ya Mafuta na Gesi, Nishati Jadidifu na Nishati safi ya kupikia.

Amesema, pamoja na kwamba wamegundua mafuta mengi, wanajipanga kuendana na sera za kidunia kwa kuwekeza katika Nishati Safi ambayo inahifadhi mazingira.

Ameongeza kuwa, Saudi Arabia inatambua juhudi zinazofanywa na Tanzania kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara katika kutekeleza Ajenda wa Nishati safi ya kupikia.

# KAPINGA ATUMIA KONGAMANO LA BIASHARA NA UWEKEZAJI SAUDI ARABIA KUNADI FURSA ZA UWEKEZAJI NCHINI

- Zaidi ya Wafanyabiasha na Wawekezaji 250 wakutana
- JNHPP yatajwa kuongeza uhakika wa uwepo wa umeme



Naibu Waziri wa Nishati Judith Kapinga(kushoto) na Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba (kulia) wakimsikiliza mgeni rasmi hayupo pichani wakati wa Kongamano la Wafanyabiashara na Wawekezaji linalofanyika Mjini Riyadh nchini Saudi Arabia tarehe 18 na 19 Desemba 2024.

Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga amesema Kongamano la Wafanyabiashara na Wawekezaji nchini Saudi Arabia litaongeza uwekezaji kwenye Sekta ya Nishati nchini kutokana na Tanzania kuzinadi fursa zilizopo kwenye maeneo mbalibali ikiwemo Gesi Asilia, umeme na Nishati Safi ya Kupikia.

Kapinga amesema hayo katika Kongamano la Wafanyabiashara na Wawekezaji zaidi ya 250 kutoka Tanzania na Saudi Arabia linalofanyika tarehe 18 na 19, Disemba, 2024 katika Mji wa Riyadh nchini Saudi Arabia.

Amesema Kongamano hilo ni muhimu kwa upande wa Wizara ya Nishati na nchi kwa ujumla kwa kuwa linatangaza fursa zilizopo nchini katika uwekezaji kupitia Sekta ya Nishati ikizingatiwa kuwa kwa sasa Tanzania inavyanzo vingi vya kuzalisha umeme mwingi na wa uhakika likiwemo Bwawa la Julius Nyerere ambalo litazalisha jumla ya Megawati 2,115.

" Kongamano hili litaendelea pia kujenga mahusiano mazuri kati ya Tanzania na Wadau kutoka Saudi Arabia katika Sekta ya Nishati." Amesema Kapinga

Akifungua Kongamano hilo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mhe. Kitila Mkumbo, aliwakaribisha wawekezaji kuwekeza nchini na kueleza kuwa Tanzania ina fursa nyingi za uwekezaji katika Sekta mbalimbali kupitia Sera nzuri, Misingi imara na Rafiki kwa wawekezaji iliyowekwa.

Aliwakaribisha wawekezaji hao kuwekeza katika nyanja mbalimbali ikiwemo Nishati, Madini, Viwanda, Biashara, Kilimo, Miundombinu pamoja na Uchumi wa Buluu.

Dkt. Mkumbo alieleza kuwa Sekta ya Uwekezaji nchini kwa sasa inakua kwa kasi kubwa, ambayo imechagizwa na Sera nzuri zilizopo chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa lengo la kuhakikisha kuwa wawekezaji wengi wanakuja kuwekeza nchini ili kukuza uchumi na kuitangaza Tanzania kote ulimwenguni.


Kwa upande wake Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Dkt. Mah'd Juma Abdalla amewaasa watanzania wanaoshiriki kongamano hilo kutumia vyema fursa hiyo kuitangaza vyema nchi yao na kutanua wigo wa biashara zao kwa kuwa nafasi hizo ni aghalabu kupatikana.



Naibu Waziri wa Nishati Judith Kapinga(katikati)akipokea tuzo kwa ajili ya ushiki wa Wizara ya Nishati katika Kongamano la Wafanyabiashara na Wawekezaji linalofanyika Mjini Riyadh nchini Saudi Arabia tarehe 18 na 19 Desemba 2024. Kulia ni Waziri Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji Profesa.Kitila Mkumbo na Waziri wa Madini, Antony Mavunde(kulia).



Naibu Waziri wa Nishati Judith Kapinga(katikati), Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Selemani Jaffo(nne kushoto), Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba(wa tatu kushoto), Waziri wa Madini Antony Mavunde(kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja katika Kongamano la Wafanyabiashara na Wawekezaji



Maafisa kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo nchini yake walioshiriki Kongamano la wafanyabiashara na Uwezaji linalofanyika Mjini Riyadh nchini Saudi Arabia tarehe 18 na 19 Desemba 2024 Oscar Kashaigire na Maafisa wengine.

Amesema kila mshiriki ahakikishe anatimiza lengo lililompeleka katika nchi hiyo ili aweze kupata matokeo chanya katika sekta yake baada ya kongamano hilo kumalizika.

Mawaziri mbalimbali wanaohudhuria Kongamano hilo ni Waziri wa Viwanda na Biashara Dkt. Selemani Jaffo, Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Madini, Antony Mavunde na Naibu Waziri wa nchi Ofisi ya Rais anayeshughulikia Ajira na Uwekezaji Zanzibar, Sharif Ali Sharif.

Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Taasisi zake wanaoshiriki Kongamano hilo ni Kamishna Msaidizi wa Petroli, Mhandisi Joyce Kisamo, Mkurugenzi Msaidizi wa Sera, Utafiti na Ubunifu, Oscar Kashaigiri na Meneja wa Biashara ya Mafuta wa kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Baraka Nyakutonya.

# DKT. KAZUNGU AKAGUA MRADI WA NJIA YA KUSAFIRISHA UMEME KUTOKA JNHPP HADI CHALINZE

- Apongeza kazi kubwa iliyofanyika katika kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme nchini.
- Mradi wafikia asilimia 97.38



Kaimu Kamishna Msaidizi wa Umeme ambaye pia ni Mratibu wa mradi wa kufua umeme wa JNHPP Mhandisi Christopher Bitesigirwe (wa tatu kulia) akitoa maelezo kwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt.Khatibu Kazungu (wa pili kulia) wakati alipotembelea mradi wa kituo cha kusafirisha umeme na kupoza umeme Cha Chalinze tarehe 28 Desemba 2024,

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. Khatibu Kazungu ametembelea mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze na kituo Cha kupoza umeme Cha Chalinze kwa ajili ya kukagua hatua ya utekelezaji wa mradi.

Akiwa katika eneo la mradi, Chalinze mkoani Pwani, Dkt. Kazungu ametembelea maeneo yote ya mradi huo na kushuhudia kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO).

Dkt. Kazungu amesema kuwa utekelezaji wa mradi huo ambao umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa Kilovoti 400 kutoka JNHPP hadi Chalinze yenye urefu wa kilomita 160 na ujenzi wa kituo

cha kupoza umeme Cha Chalinze ambacho kinahusisha ufungaji wa transfoma sita zenye uwezo wa MVA 250 kila moja ni kiunganishi kikubwa katika kuhakikisha umeme unafika pande zote za nchi.

“ Kakamilika kwa mradi huu kutasaidia umeme kutoka JNHPP kufika pande zote zilizokusudiwa. TANESCO msimamieni Mkandarasi akamilishe kazi kwa ufanisi kwani umeme ni maisha na uchumi ambao ukipatikana utafungua fursa za viwanda ambazo zitainua maisha ya mtu mmoja mmoja na kukuza uchumi nchini.” Amesema Kazungu

Amesema malengo ya mradi huo ni pamoja na usafirishaji wa umeme ( 2,115 MW) utakaozalishwa katika Bwawa la JNHPP na kuufikisha Chalinze,vile vile lengo la pili ni kuwa na kituo Cha kupoza umeme Cha Chalinze kwa ajili ya kupokea umeme kutoka Bwawa la JNHPP na kuboresha upatikanaji wa umeme kwenye Gridi ya Taifa.

Ujenzi wa kituo Cha kupoza umeme cha Chalinze ulianza Mwezi Oktoba 2021 na utekelezaji wa mradi mpaka sasa umefikia asilimia 97.38, huku kazi za ufungaji wa mifumo ya kuendesha kituo zikikamilika na kwa sasa kituo kinapokea umeme unaozalishwa kutokea JNHPP na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt Khatibu Kazungu (wa kwanza kushoto) akitoa maelekezo kwa Wahandisi Wasimamizi wa Mradi wa Kituo Cha Kusafirisha Umeme na kupoza umeme cha Chalinze tarehe 27 Desemba 2024.

# NCHI ZA EAC NA SADC ZAAZIMIA KUENDELEZA TEKNOLOJIA ZA MATUMIZI BORA YA NISHATI

- Ni katika Mkutano wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati
- Dkt. Jafo asema maendeleo ya Viwanda yanategemea uwepo wa Nishati ya kutosh




Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Selemani Jafo akikabidhi tuzo za Uhamasishaji na uendelezaji wa Matumizi Bora ya Nishati kwa mmoja wadau wa Nishati wakati akifunga Mkutano wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati uliofanyika Arusha Tarehe 4 na 5 Desemba, 2024.Kulia ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dkt. Khatibu Kazungu.

Mkutano wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati uliohusisha Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliomalizika leo jijini Arusha umetoka na maazimio mbalimbali yatakayowezesha nchi za EAC na SADC kuwa na Matumizi Bora ya Nishati.

Moja ya maazimio hayo kuendeleza Teknolojia za Matumizi Bora ya Nishati ili kuwa na ufanisi katika matumizi ya nishati.

Mkutano huo uliokuwa ukifanyika jijini Arusha tarehe 4-5 Desemba 2024 umefungwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Selemani Jafo ambaye ameeleza kuwa umehusisha Watunga Sera, Sheria, Viongozi, Wataalam na Wabobezi katika masuala ya Nishati kwa lengo moja la kuwa na matumizi sahihi ya Nishati.

Dkt. Jafo amesema lengo la nchi ni kuendelea kukuza uchumi, viwanda vifanye kazi na biashara zifanyike kwa ufanisi lakini hilo litawezekana ikiwa kuna nishati ya kutosha ambayo uwepo wake unategemea usahihi katika matumizi yake.

Ameeleza kuwa, Tanzania inatilia mkazo suala la matumizi bora ya nishati ambapo kwa sasa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linaandaa viwango fanisi vya vifaa vya nishati vinavyozalishwa au kuingizwa nchi ambavyo vitawezesha nchi kutumia umeme kwa ufanisi.

Amemshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwekeza katika miradi ya Nishati ambapo uwekezaji huo amesema kwamba una maana kubwa katika kuendeleza viwanda na biashara.

Aidha, ameishukuru Wizara ya Nishati kwa kuratibu Mkutano huo wa Siku mbili kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Ubalozi wa Ireland.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. Khatibu Kazungu amesema Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Nishati imejipanga kutekeleza Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati uliozinduliwa tarehe 4 Desemba 2024 kwa kuhakikisha Mkakati huo unatekelezwa kwa kuwekewa bajeti ili nchi iweze kuwa na ufanisi katika vifaa vya nishati.

Amesema kupitia Mkutano wa REEC 2024 maazimio mbalimbali yamefikiwa ikiwemo kufanya tafiti za pamoja ili kuboresha matumizi bora ya nishati na kuihusisha kikamilifu Sekta Binafsi.

kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mhe.Selemani Kakoso amsipongeza Serikali kwa kuendesha na kusimamia mkutano wa REEC 2024 ulioleta mafanikio makubwa ikiwemo mafunzo na kubadilishana uzoefu ili kuwa na ufanisi.kwenye matumizi ya nishati.




Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Selemani Jafo akizungumza na washiriki wa Mkutano wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati ( hawapo pichani) uliofanyika Arusha Tarehe 4 na 5 Desemba, 2024.




Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Selemani Jafo akiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya Wizara ya Nishati, wakati akifunga Mkutano wa Kikanda wa Matumizi Bora ya Nishati uliofanyika Arusha Tarehe 4 na 5 Desemba, 2024.

# DKT. KAZUNGU AKAGUA MAENDELEO YA MRADI WA UMEME WA JNHPP

- Asema ni chanzo kikubwa cha ukuaji wa uchumi nchini
- Apongeza kazi kubwa iliyofanyika katika mradi huo
- Mradi wafikia asilimia



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt Khatibu Kazungu (wa Pili kulia) akikagua mradi wa kufua umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Wa Tatu kulia ni Kaimu Kamishina Msaidizi wa Umeme ambaye pia ni Mratibu wa umeme wa JNHPP, Mhandisi Christopher Bitesigirwe tarehe 27 Desemba 2024.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. Khatibu Kazungu ametembelea mradi wa kufua Umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115kwa ajili ya kukagua hatua ya utekelezaji wa mradi.

Akiwa katika eneo la mradi, Rufiji mkoani Pwani, Dkt. Kazungu ametembelea maeneo yote ya mradi huo na kushuhudia kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Wizara ya Nishati kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Dkt. Kazungu amesema kuwa mradi huo ambao sasa unaingiza zaidi ya megawati 1000 kwenye gridi ya Taifa ni chachu kubwa katika kukuza uchumi wa nchi.

“Mradi huu ni kielelezo muhimu sana katika nchi yetu kwani moja ya chachu kubwa za kukuza uchumi nchini ni matumizi ya umeme, kuna uhusiano mkubwa wa umeme na maendeleo ya kiuchumi na mifano halisi tunaiona, nchi nyingi Duniani zenye matumizi makubwa ya umeme zimeendelea sana kiuchumi, hivyo Wizara ya Nishati tutaendelea kuongeza nguvu katika kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme. Amesema Kazungu.

Aidha, amemsisitiza Mkandarasi wa mradi kumaliza kazi kwa wakati na kuwapongeza TANESCO kwa usimamizi wa mradi huo.

Vilevile ameitaka TANESCO kugeukia vyanzo vingine vya umeme kama Jotoardhi na Jua ili kuhakikisha kunakuwa na umeme wa kutosha kwa matumizi ya ndani ya nchi na pia kuwezesha biashara ya umeme nje ya nchi.

Maendeleo ya jumla ya mradi wa JNHPP hadi kufikia tarehe 30 Novemba 2024 yamefikia asilimia 99.55 na kuingiza 1,175 MW katika gridi ya Taifa.

# BARAZA LA WAFANYAKAZI WIZARA YA NISHATI LAKUTANA JIJINI ARUSHA

- Bajeti ya Wizara 2024/2025 na Majukumu ya Wizara kujadiliwa kwa kina
- Dkt.Kazungu afungua Mkutano
- Asema stahiki za kisheria za Watumishi zinapewa kipaumbele
- TUGHE yapongeza ushirikiano uliopo kati ya Menejimenti na Wafanyakazi



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt.Khatibu Kazungu akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi jijini Arusha tarehe 6 Desemba 2024.

Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Nishati limekutana jijini Arusha kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Wafanyakazi wa Wizara husika.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt.Khatibu Kazungu amefungua Mkutano wa Baraza hilo jijini Arusha, tarehe 06 Desemba, 2024 na kueleza kuwa kufanyika kwa Mkutano huo ni utekelezaji wa sheria mbalimbali zinazoelekeza waajiri wote kuhakikisha wanaunda mabaraza ya wafanyakazi mahala pa kazi.

"Kufanyika kwa mikutano hii ya Mabaraza ya Wafanyakazi kunatokana na agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la mwaka 1970, Sheria ya Utumishi wa Umma sura na.298 ya mwaka 2002 na kanuni zake za mwaka 2022 ikisomwa kwa pamoja na sheria ya majadiliano kazini ya mwaka 2004 pamoja na sheria ya ajira na mahusiano kazini ya mwaka 2004." Amesema Dkt. Kazungu

Ameeleza kuwa, Mkutano huo wa Sita wa Baraza la Wafanyakazi utakuwa na majukumu mbalimbali ikiwemo kupokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/25 kuanzia mwezi Julai-Desemba 2024, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2024 (Julai-Desemba) na kupitia Mpango wa Mafunzo wa Wizara wa mwaka 2024/25-2026/27.

Ameongeza kuwa, katika Baraza hilo pia itatolewa taarifa kuhusu kiasi cha fedha kilichopitishwa na Bunge kwa mwaka 2024/2025, fedha zilizopokelewa, majukumu yaliyotekelezwa, changamoto zilizojitokeza na mbinu zilizotumika kutatua changamoto hizo ili kuweza kusonga mbele kwa mafanikio na ufanisi zaidi.

Amesema kuwa kwa mwaka 2024/2025 fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa Wizara ni sh trilioni



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt.Khatibu Kazungu pamoja na viongozi wengine wakiimba wimbo wa mshikamano katika Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi jijini Arusha tarehe 6 Desemba 2024. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa na kulia kwake ni Katibu wa Baraza Wizara ya Nishati, Cosmas Kiguli.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt Khatibu Kazungu (wa Pili kulia) akikagua mradi wa kufua umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Wa Tatu kulia ni Kaimu Kamishina Msaidizi wa Umeme ambaye pia ni Mratibu wa umeme wa JNHPP, Mhandisi Christopher Bitesigirwe tarehe 27 Desemba 2024.

1.8 huku sh. trilioni 1.7 ikiwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida yakiwa ni sh.bilioni 88.8.

Dkt. Kazungu amesema kuwa, Wizara ya Nishati imeendelea kuhakikisha kwamba bajeti inazingatia stahiki za kisheria za watumishi kama vile malipo ya nauli za likizo na posho ya kujikimu.

Kwa upande wake, Meshack Lugeiyamu kutoka TUGHE Taifa ameipongeza Menejimenti ya Wizara ya Nishati kwa kuwa na ushirikiano chanya na Wafanyakazi wa Wizara ambao amesema kuwa kwa kiasi kikubwa unaimarishwa na vikao vinavyofanyika mara kwa mara kati ya pande hizo mbili ambavyo ni sehemu ya kupata mrejesho wa masuala mbalimbali kuhusu watumishi.

Vilevile amesema Wizara ya Nishati ni ya kuigwa mfano kutokana na kufanya mikutano ya Baraza la Wafanyakazi kwa mujibu wa taratibu na kalenda.

Katika Mkutano huo wa sita wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Nishati, alitambuliswha Mwenyekiti Mpya wa TUGHE Tawi la Nishati ambaye ni Bi. Zuena Msuya.

Kaulimbiu ya Mkutano huo ni Matumizi ya Nishati ya Safi ya Kupikia kwa Maendeleo Endelevu ya Tanzania

# SERIKALI BEGA KWA BEGA NA WAFANYABIASHARA KUTATUA CHANGAMOTO ZAO

- Rais Samia Apongezwa Kuifungua Nchi Kiuchumi
- Dkt. Biteko Awahimiza Wafanyabiashara Kulipa Kodi Kwa Maendeleo ya Nchi
- TCCIA Yaendelea Kuwa Daraja la Wafanyabiashara wa Tanzania, Yafungua Ofisi China, London na Uturuki
- Serikali Yapongezwa Kwa Kuwekeza Kwenye Miundombinu




Serikali imesema itaendeleza jitihada zake za kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara kwa lengo la kuboresha shughuli za biashara, uwekezaji na kukuza uchumi wa nchi.

Sambamba na kushirikiana na sekta binafsi ili kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara nchini ikiwa ni pamoja kujenga na kuimarisha miundombinu kwa ajili ya usafiri na usafirishaji.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko Desemba 6, 2024 jijini Dar es salaam wakati akifungua Kongamano la Majadiliano ya Biashara na Uwekezaji kati ya Serikali na Sekta Binafsi Mwaka 2024 na Mkutano Mkuu wa 49 wa Mwaka 2024 wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Dkt. Biteko ameeleza umuhimu wa sekta binafsi na kusema kuwa nchini Tanzania na Afrika kwa ujumla inakisiwa kuwa vijana zaidi ya bilioni 12 wanaingia katika soko la ajira na kati yao asilimia 70 wanategemea sekta binafsi ndio maana Serikali imeendelea kushirikiana na kutatua changamoto za sekta binafsi.

“ Hivi karibuni mlitoa malalamiko kadhaa ikiwemo ya kukwamisha shughuli za biashara na Serikali imeyatatua kwa kushirikiana nanyi pamoja na wadau wa maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi,” amesema Dkt. Biteko.

Ametaja baadhi ya jitihada zilizofanywa na Serikali za kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini kuwa ni pamoja na kufanywa marekebisho ya sheria na kanuni 55 na sheria zingine 16 na kanuni zake zinaendelea kufanyiwa kazi.

Amesisitiza “ Serikali imeondoa mwingiliano wa majukumu na kuanzisha mamlaka mfano sasa tuna Mamlaka ya Chakula na Dawa (TMDA) ili kurahisisha shughuli zenu. Pia, imepunguza idadi ya muda wa kupata huduma kutoka siku 14 hadi tatu na kutoka siku saba hadi tatu za kusafirisha mizigo kutoka Dar es salaam hadi Tunduma.”

Pamoja na hayo Dkt. Biteko amefafanua kuwa Wakala wa Usalama Mahala Pa kazi (OSHA) imepunguza tozo 16 za biashara ambazo kupitia hizo Serikali inapoteza mapato kiasi cha shilingi bilioni 37 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi na jitihada za Rais Samia za kuboresha mazingira ya biashara nchini.

Fauka ya hayo, amezungumzia viashiria vya ukuaji wa uchumi na kusema kuwa kumekuwepo na ongezeko la mahitaji ya nishati ya umeme ambapo awali hayakuwahi kuzidi megawati 219 kwa mwaka na kuwa mwaka 2024 mahitaji ni megawati 420.

“ Mkifanyabiashara maana yake mahitaji ya nishati ya umeme yanaongezeka na hii ni kwa sababu viwanda vingi vimejengwa na uchumi unachangamka. Tunaanza kuona wananchi wanatumia umeme megawati 52 na viwanda vinatumia megawati 48 hii ni kiashiria kuwa uchumi unaendelea kukua vizuri,” amebainisha Dkt. Biteko.

Vilevile, amewaasa wafanyabiashara nchini kulipa kodi kwa hiari ili Serikali iweze kutekeleza ujenzi wa miradi mbalimbali itakayosaidia utoaji huduma za kijamii kwa wananchi na kuchochea maendeleo huku akiwataka kuzalisha malighafi na bidhaa zenye ubora zitakazovutia masoko na kutoa ajira kwa watu.

“Nchi yetu tutaijenga wenyewe na tuambiane ukweli kwamba kulipa kodi ni wajibu wetu, kwa mikataba hii iliyowekwa saini hapa leo TCCIA muwe mawakala wa kutoa elimu ya mlipa kodi kwa wananchi ili watu waone heshima ya kulipa kodi,” amesema Dkt. Biteko.

Ameendelea kuwakaribisha wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nje ya nchi kuja kuwekeza nchini huku akivitaka vyama vya kisekta kuepuka migogoro na kusisitiza upendo, ushirikiano na mshikamano miongoni mwao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. John Lukuvi amesema kusanyiko hilo la zaidi ya wafanyabiashara na wakulima 300 kutoka nchi nzima ni muhimu na kuwa kupitia jukwaa hilo Serikali itaendelea kushirikiana nao ili kukuza sekta binafsi nchini.

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mhe. Edward Mpogolo amesema kuwa Mkoa huo umekuwa na ushirikiano mzuri na TCCIA katika shughuli mbalimbali.

“Wafanyabiashara hawa wamekuwa wakipongeza jitihada za Rais Samia kwa kupunguza msongamano wa meli bandarini, kuboreshwa kwa miundombinu wezeshi ya viwanda mfano zaidi ya shilingi trilioni moja imetolewa katika miradi ya barabara ya DMDP na sasa umeme uko wa kutosha na wanaendelea kufanya biashara vizuri,” amesema Mpogolo.

Rais wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Vicent Minja kwa niaba ya wafanyabiashara nchini amempongeza Rais Samia kwa jitihada zake za kuifungua nchi na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara Tanzania na hivyo kusaidia biashara kufanyika kwa utulivu.

Amesema taasisi yake ina ofisi katika nchi za China, Uturuki na Uingereza na hivyo inarahisisha kuunganisha wafanyabiashara wa Tanzania na nchi mbalimbali.

“Tunaishukuru Serikali kwa kurahisisha maendeleo ya biashara katika Bandari ya Dar es salaam sasa meli zikija na mizigo zinapakuwa ndani ya siku chache, pia tunamshuru Rais Samia kwa kuunda tume ya kushughulikia masuala ya kodi,” amesema Minja.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Oscar Kissanga amesema kuwa taasisi yake inalenga kuunganisha wadau wa biashara na kukuza sekta ya biashara na kilimo nchini.

"Katika kipindi cha miaka 36 TCCIA imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuimarisha ushindani na kuvutia wadau wa ndani na nje ya nchi," amesema Kissanga

Ameongeza kuwa lengo TCCIA ni kuhakikisha sekta binafsi inashiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo endeleo na kujenga uchumi imara huku akimpongeza Rais Samia kwa jitihada zake za kuhakikisha kunakuwepo na ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa nchi.

Kissanga ametaja baadhi ya utekelezaji wa shughuli za TCCIA katika kipindi cha mwaka 2024 kuwa kutoa mafunzo ya kuelimisha Watanzania kuhusu Soko Huru la Afrika kutoka katika mikoa nane, imesafirisha shehena za bidhaa mbalimbali katani ikiwa ni asilimia 70 ya shehena yote.

Vilevile, imefanya ukaguzi wa viwanda 37, na kufanya Jukwaa la Biashara ya Korosho Tanzania na kuleta nchini zaidi ya kampuni 100. Sambamba na kuzisaidia kampuni za Tanzania kupata fursa za uwekezaji na masoko kutoka nchi mbalimbali duniani.

Mkurugenzi Mkazi wa Kampuni ya Trademark Afrika, Elibariki Shammy amesema taasisi yake inalenga kuisaidia Watanzania na Afrika kwa ujumla ili iweze kufanyabiashara na dunia na kuwa ina wadau kutoka sekta ya umma na binafsi na hivyo wanashukuru kwa kuendelea kuaminiwa katika kutekeleza shughuli zao.

Aidha, kupitia Kongamano hilo Dkt. Biteko ameshuhudia utiaji saini wa baadhi ya mkataba ikiwemo mkataba kuwezesha kufanya kazi pamoja kati ya Serikali na sekta binafsi, ushirikiano wa biashara kati ya TCCIA na Chuo Cha Biashara (CBE) ambapo CBE inatarajia kuwa na mitaala ya biashara ya wanagenzi na hivyo ushirikiano huo utasaidia kufikia wafanyabiashara watakaosaidia kufundisha wanafunzi.

Mkataba mwingine uliowekwa saini ni wa kutekeleza masuala mbalimbali ikiwemo kuhamasisha wanachama wa TCCIA kulipa kodi kwa hiari kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kurahisisha ulipaji kodi na kutoa elimu ya namna kiwango na muda wa kulipa kodi.

Kongamano hilo limeongozwa na kaulimbiu "Kuongeza Ufanisi wa Majadiliano na Ushindani wa Mauzo ya Nje kwa Ustawi wa Uchumi" limehudhuriwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mhe. Prof. Kitila Mkumbo, Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Selemani Jafo, viongozi mbalimbali pamoja na wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya nchi.



# BENKI YA DUNIA, SADC ZAMPONGEZA RAIS SAMIA UTEKELEZAJI MIRADI YA MAENDELEO

- Dkt. Biteko asema nia njema ya Rais Samia iungwe mkono kuleta maendeleo kwa Watanzania
- Ampongeza Mbunge Kiswaga kwa Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akihutubia wananchi katika Mkutano Mkuu wa Jimbo la Magu wa kutoa taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha Mwaka 2020-2024 uliofanyika Wilayani Magu, Desemba 23, 2024.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini ikiwemo Wilaya ya Magu.

Amesema hayo Desemba 23, 2024 wilayani Magu mkoani Mwanza katika Mkutano Mkuu Maalum ambapo taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu Jimbo la Magu kwa mwaka 2020 hadi 2024 iliwasilishwa.

“Mhe. Rais amefanya kazi kubwa ya kupigiwa mfano na anastahili pongezi, nataka niwaambieni kuna watu wengine wanaumia tukimpongeza Rais Samia, lakini wajue hatutoi pongezi hizi peke yetu hata huko duniani kwa mfano Benki ya Dunia na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wanampongeza kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa asilimia 5.1,” amesema Dkt. Biteko.

Amesema pia kuwa Rais Samia ana nia njema na anataka kuona Watanzania wanapata maendeleo.

Ameongeza kuwa maendeleo katika Jimbo la Magu hayakuja kwa bahati mbaya isipokuwa kwa mipango na hivyo anawapongeza wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Magu kwa tamko la pongezi kwa Rais Samia kwa kuwapa fedha kiasi cha shilingi 143.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Ametaja baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Serikali “ Barabara za lami zimeunganisha mikoa yote nchi nzima, tuna ndege za abiria na mizigo, tumejenga shule nyingi na sasa tunajenga shule za kata maeneo mbalimbali



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda akitoa taarifa kwa wananchi katika Mkutano Mkuu wa Jimbo la Magu wa kutoa taarifa ya Mkoa huo katika Mkutano ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha Mwaka 2020-2024 uliofanyika Wilayani Magu, Desemba 23, 2024.

nchini. Maendeleo yanaonekana kwa macho na sisi ni kazi yetu kusema haya kwa wivu mkubwa,"

Kuhusu umeme Dkt. Biteko amesema katika kijiji kimoja pekee ambacho hakina umeme, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 600 kwa ajili ya kupeleka umeme huku mipango ya kupeleka umeme katika kisiwa ikiendelea.

Aidha, amempongeza Mbunge wa Jimbo la Magu, Mhe. Kiswaga kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo.

Dkt. Biteko amesema "CCM ni chama kiongozi hivyo wanaCCM tembeeni kifua mbele hubirini yanayofanywa na chama chenu waonesheni watu maendeleo yaliyotokea msiwapuuze,"

Pamoja na hayo amempongeza Mhe. Kiswaga kwa kusimamia miradi ya maendeleo huku akiwaasa wanachama wa CCM kushirikiana na viongozi kwa ngazi zote ili kuendelea kuimarisha chama huku akiwapongeza kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Jimbo lao.

Mbunge wa Jimbo la Magu, Mhe. Boniventura Kiswaga wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu Jimbo la Magu kwa mwaka 2020 hadi 2024 amesema Serikali ya Rais Samia imeendelea kuwapa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwemo shilingi bilioni 78 kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraja.

Amebainisha kuwa Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) wametoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 48 kwa ajili ya kujenga daraja la Simiyu.

"Kwenye sekta ya maji tumepokea shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kujenga tanki lenye lita za ujazo milioni 5 litakalohudumia kata 14," amesema Mhe. Kiswaga.

Amesema Rais Samia katika bajeti ya mwaka huu ametenga fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwemo ya kutoa maji Ihale, kujenga tanki lenye ujazo wa lita milioni 2 pamoja na mradi wa kuchimba visima virefu.

Katika upande wa sekta ya elimu, amesema "Tumepokea fedha kiasi cha shilingi bilioni zaidi ya 31, tumemaliza ujenzi wa sekondari za kata sasa tunaendelea kujenga sekondari za vijiji nia yetu ni kumpelekea maendeleo kwa wananchi,"

Vilevile, katika afya wilaya hiyo imepokea shilingi bilioni 10 ambapo wamekarabati na kujenga vituo vipya vya afya.

Aidha, ameshukuru Rais Samia kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Jimbo lake.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda amepongeza Mhe. Kiswaga kwa kuandaa mkutano utakaotoa fursa kwa wananchi kuelezwa yale aliyotekeleza katika kuwaletea maendeleo.

"Kwa miaka mitatu Serikali inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan imeleta shilingi trilioni 5.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo hapa Magu,"

Mhe. Mtanda amesema baada ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, CCM Magu imeshinda katika vijiji 78 kati ya 82 na katika vitongoji 508, imeshinda vitongoji 484 huku akiwataka wananchi kudumisha amani mara baada ya uchaguzi huo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Magu, Enos Kalambo amesema kuwa Rais Samia na Mbunge wao Kiswaga wamefanyakazi kubwa ya kuwaletea maendeleo katika wilaya hiyo hivyo wananchi waendelee kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao.

# WAWEKEZAJI WAKARIBISHWA KAGERA

- Dkt. Biteko asisitiza teknolojia itumike uchakataji zao la ndizi
- Dkt. Biteko ahimiza uwekezaji viwanda vya kuongeza thamani mazao ya uvuvi na ufugaji
- Kagera yaongoza kwa uzalishaji zao la ndizi nchini kwa asilimia 60
- Mradi wa Mashamba Makubwa ya Kahawa Kagera kunufaisha watu 10,000



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, akizungumza katika Tamasha la Pili la Uwekezaji Mkoani Kagera.

Wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi wamekaribishwa kuwekeza mkoani Kagera kufuatia hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ambazo mkoa wa huo umefikia ikiwa ni pamoja na mipango ya maendeleo na fursa nyingi za uwekezaji zilizopo.

Mkoa wa Kagera ni wa pili kwa uzalishaji wa samaki na fursa ya uvuvi nchini ukitanguliwa na Mkoa wa Mwanza fursa ambayo inawanufaisha wakazi wake kwa kuwapatia ajira, lishe bora, kipato na maendeleo ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa makazi bora kutokana na shughuli za uvuvi.

Akizungumza Desemba 19, 2024 katika Uwanja wa Kaitaba wilayani Bukoba mkoani Kagera wakati aliposhiriki katika Tamasha la Pili la Uwekezaji la mkoa huo ikiwa sehemu ya Wiki ya Tamasha

la Ijuka Omuka (Kumbuka Nyumbani), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ametoa wito kwa wananchi wa mkoa huo kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani mazao ya uvuvi, viwanda vya kutengeneza zana za uvuvi kama nyavu, kamba, vifaa vya kujiokolea na mashine za boti badala ya kuagiza vifaa hivyo kutoka nje ya nchi.

Dkt. Biteko amesema kuwa Mkoa wa Kagera unaongoza kitaifa kuwa na ranchi 6 za mifugo kati ya ranchi 15 zilizopo nchini. Ametaja ranchi hizo kuwa ni Missenyi, Mabale, Kikulula, Mwisa II, Kitengule na Kagoma.

Ameendelea kusema kuwa mkoa huo kupitia halmashauri zake zote umetenga jumla ya hekta 345,430.97 kwa ajili ya malisho ya mifugo ambapo uwepo wa maeneo hayo ya malisho na ufugaji yanatoa fursa kubwa ya uwekezaji kwa kuanzisha ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa nyama na maziwa ili kuvutia uanzishwaji wa viwanda vya kuchataka nyama na maziwa hasa katika maeneo yenye ranchi za Taifa.

" Naiona Kagera inakwenda kukua kwa kasi kubwa sana na nitumie fursa hii kuwaomba na kuwaalika wawekezaji kote nchini na nje ya nchi kuja kuwekeza Kagera kutokana na fursa zilizopo kwani mazingira ya uwekezaji ni mazuri na uongozi wa mkoa umejipanga vyema kuwapokea na kuwahudumia kwa viwango," amesema Dkt. Biteko

Ameongeza kuwa Mkoa wa Kagera pia unaongoza kwa uzalishaji wa zao la ndizi kwa wastani wa tani milioni 2.4 kati ya tani milioni 3.6 zinazozalishwa sawa na asilimia 60 ya uzalishaji wa zao hilo nchini. Kwa wastani zao la ndizi mkoani humo linawaingizia wakulima kati ya shilingi bilioni 240 – 300 kwa mwaka, hivyo kuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa mkoa na Taifa kwa ujumla.

Pia, Dkt. Biteko amesema bado ipo fursa ya kuwekeza kwenye teknolojia na miundombinu ya uchakataji wa zao la ndizi ili kuongeza thamani na kuzalisha bidhaa nyingine zinazotokana na zao la hilo.

"Ninafahamu kwamba, mkoa umebuni na kuanzisha mradi wa Mashamba Makubwa ya Kahawa yenye ukubwa wa ekari 10,000. Mradi ambao unalenga kuwanufaisha watu wapatao 10,000 wakiwemo vijana na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2024 – 2027. Kwa kuanzia tayari shamba lenye ukubwa wa ekari 400 katika Kijiji cha Makongora wilayani Muleba ambapo kila kijana amegawiwa ekari moja ya shamba lililoandaliwa na kupewa miche bure," amesema Dkt. Biteko.

Aidha, lengo la mradi huo likitajwa kuwa ni kuongeza ajira kwa vijana, pato la mtu mmoja na pato la mkoa pamoja na kuongeza pato la halmashauri kupitia ushuru wa zao la kahawa na kuliingizia Taifa fedha.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mhe. Fatma Mwassa amesema kuwa Tamasha la Ijuka Omuka (Kumbuka Nyumbani), limelenga kuwakutanisha pamoja wakazi wa Kagera na kuibua fursa za uwekezaji mkoani humo.

Amesema kuwa kupitia tamasha hilo wanautangaza Mkoa wa Kagera licha ya kutokuwepo kwa jitihada za kufanya hivyo hapo awali ili wananchi wa mkoa huo kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi kuvutiwa na fursa zilizopo na kwenda kuwekeza katika sekta mbalimbali.

Tamasha la Ijuka Omuka 2024 limeanza Desemba 18, 2024 na linatarajiwa kuhitimishwa Desemba 21, 2024. Tamasha hilo limesheheni matukio mbalimbali ikiwemo maombezi kwa Mkoa wa Kagera na Taifa, Kongamano la Uwekezaji, maonesho ya biashara, tamasha la utamaduni, maonesho ya mavazi ya asili, mashindano ya pikipiki na mechi kabambe ya mpira wa miguu Desemba 21, 2024 kati ya Klabu ya Simba na Kagera Sugar katika Uwanja wa Kaitaba mkoani humo.

# KUWENI BARAKA, SIO KITUNGUU KUWATOA MACHOZI WENGINE - DKT. BITEKO

- Amwakilisha Rais Samia hafla ya kutabaruku kanisa SDA- Magomeni
- Ataka watu kutengenezeana furaha badala ya kuumizana
- Ahimiza Mshikamano wa Taifa ili kuleta maendeleo




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akipokea zawadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan wa alipomwakilisha kuwa mgeni maalum katika Hafla ya Kutabaruku Jengo la Kanisa la Waadventista Wasabato, Magomeni 17 Disemba, jijini Dar es salaam (Picha na Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Naziri Mkuu)

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewataka Watanzania kujenga misingi ya kusaidiana kuheshimiana na kuvumiliana ili kufanikisha malengo wanayojiwekea kimaendeleo.

Dkt. Biteko ametoa rai hiyo leo Desemba 15, 2024 Jijini Dar es Salaam alipomwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgeni maalum katika Hafla ya Kutabaruku Jengo la Kanisa la Waasventista Wasabato, Magomeni.

Amewahimiza waumini na Watanzania kwa ujumla kuboresha huduma za jamii na kuwekeza katika mipango itakayowezesha kukidhi mahitaji na kupata Taifa endelevu.

“ Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan siku zote amekuwa akisisitiza maridhiano, uhimilivu, mabadiliko na kuimarisha amani yetu ili jamii iweze kupata maendeleo na kustawi” amesema Dkt. Biteko

Aidha, amewataka waumini kuendeleza moyo wa kujitolea kwa ajili ya uwekezaji na ujenzi wa miundombinu ya maendeleo kama vile kanisa na miradi mingine ya kijamii.

Amesema, Serikali itaendelea kutoa ushirikiano wake kuhakikisha kwamba misingi ya

malezi na ushirikiano inayowekwa inafanikiwa.

" Wametajwa baadhi ya watu waliofanikisha ujenzi wa kanisa hili la Magomeni, lakini pia wapo ambao hawakutajwa kwa kuwa hawakuwa tayari kutajwa na hii ndiyo sababu kwao kutotajwa, sasa tuanze upya kila mmoja ajitahidi kufanya jambo la kheri kwa mwenzie badala ya kumuumiza," ameongeza kuwa tuwe baraka kwa watu wengine na sio Kitunguu cha kuwatoa watu machozi machoni" amesisitiza Dkt. Biteko

Kwa upande wake, Mch. Dkt. Joel Okindo, Msaidizi wa Mwenyekiti wa Divesheni ya Mashariki na Kati amewaka waumini kujenga moyo wa kujitolea katika masuala ya maendeleo ili kutimiza azima ya uumbaji.

Amesema ujenzi wa Kanisa la SDA - Magomeni ulianza takribani miaka 12 iliyopita na ujenzi huo umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 kutokana na michango ya waumini, wafadhili na viongozi mbalimbali.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila ametumia jukwaa hilo kutoa ufafanuzi kuhusu madai ya mtu mmoja anayedaiwa kutekwa ambapo amesema mtu huyo alitumia mbinu hizo baada ya kuuza gari alilokuwa ameazima.

" Mhe. Naibu Waziri Mkuu, Dar es Salaam ni salama na huyu mtu anayedaiwa kutekwa ni kwamba "amejiteka" baada ya kuazima gari na kuliuza, Gari tayari tunalo na huyo mtuhumiwa atatokea hadharani hivi karibuni kuelezea kilichotokea." amesema Chalamila.

# TUWAINUE WABUNIFU WAZAWA KUWANADI KIMATAIFA - DKT. BITEKO

- Asisitiza Mifumo iboreshwe kuakisi Maendeleo
- Serikali kuweka Mazingira wezeshi kwa wadau wa STARTUPs



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akipokea zawadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan wa alipomwakilisha kuwa mgeni maalum katika Hafla ya Kutabaruku Jengo la Kanisa la Waadventista Wasabato, Magomeni 17 Disemba, jijini Dar es salaam (Picha na Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Naziri Mkuu)

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa pamoja na jitihada za kuwainua wabunifu wawekezaji nchini, bado kuna umuhimu mkubwa wa kuwawezesha wabunifu wetu kukua zaidi ndani na nje ya mipaka ya nchi.

Dkt. Biteko amesema hayo Desemba 16, 2024 Jijini Dar es Salaam alipomwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kufungua Kongamano la Uwekezaji wa Kampuni Bunifu (STARTUPs)

Amesema kuwa Tanzania imerekebisha mifumo mingi ili kuwezesha ubunifu na uwekezaji wa moja kwa moja nchini kuleta maendeleo, suala ambalo tumeona likifanikiwa na kwahiyo linahitaji kupaliliwa na kuungwa mkono kwa matokeo chanya.

"Nimewasikilizawanakongamano na kupitia majadiliano haya ni

wazi kwamba bado kuna namna ya kuboresha zaidi mifumo yetu ya usimamizi na utawala ili kuhakikisha Wabunifu wanapata nafasi nzuri zaidi." amesema na kuongeza kuwa, Tunatamani kuona Watanzania wanashiriki katika kukuza uchumi wa nchi yao na pengine kuazimwa katika nchi nyingine." amesema Dkt. Biteko

Amesema wapo baadhi ya Watanzania wanaofanya shughuli zao nje ya Nchi ambao wanaiwakilisha vema Tanzania kutokana na kufanya kazi kwa kuzingatia misingi iliyowekwa katika nchi hizo na hivyo kuwataka wabunifu wawekezaji kuiga mfano huo.

Aidha, Dkt. Biteko amesema kuwa Maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan yako wazi na kwa nyakati mbalimbali amekuwa akijipambanua kuhusu uwezeshaji wa makundi mbalimbali wakiwemo wabunifu wawekezaji.

"kwa kutekeleza maono ya Rais, ni muhimu kuwasikiliza, kuwaamini na kufanyia kazi maoni na bunifu zao ili kuboresha mazingira yatakayo wawezesha kutekeleza Bunifu zao na kupata fursa ndani na nje ya Nchi".

Naye, Naibu Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Mhe. Stanslaus Nyongo akimwakilisha Waziri wa Wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo amesema Serikali imekuwa ikizingatia suala la uwezeshaji kwa Wabunifu Wawekezaji ikiwa ni pamoja na kupokea maoni yao kupitia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Nyongo ameongeza kuwa, Serikali imeboresha mazingira ya biashara kwa kupunguza gharama za biashara ili kuwawezesha wabunifu kutimiza ndoto zao.

Kwa upande wake, Waziri Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Jerry Silaa amesema Wizara imeandaa mazingira ya kuwawezesha Wabunifu kufanya majaribio ya kazi zao kupitia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Amesema Serikali imejenga vituo vya ubunifu vinane (8) katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuwawezesha Wabunifu kujiandaa na hatimaye kupata ajira katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TSA, Zahoro Muhaj amemshukuru Rais Samia kwa maono yake ya kuwatambua na kuwawezesha wabunifu ili waweze kuchagiza maendeleo ya nchi.

" Tunaomba salam zetu zifikishwe kwa Mheshimiwa Rais, ambaye amekuwa akitubeba na kusafiri nasi katika nchi mbalimbali ili tupate uzoefu na kukua kama mtu kama mtu mmoja mmoja na baadae kama Taifa," amesema Muhaj.

Kwa upande wake, Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Nelson Bonephace ameishukuru Serikali kwa jitihada za kuwawezesha wabunifu wawekezaji kukua.

Amesema katika kipindi cha mwaka 2020 hadi sasa zaidi ya dola za kimarekani Milioni 49 zimetolewa ambazo zinatumika kujenga Kampasi mpya za Kagera, Zanzibar na Lindi



# WAHASIBU AFRIKA WAASWA KUSIMAMIA UKWELI WA TAALUMA YAO

- Dkt. Biteko Amwakilisha Rais Samia Kufunga Mkutano AAAG
- Asema Afrika Inawategemea Wahasibu Kunufaika na Utajiri wake
- Asisitiza Matumizi ya Teknolojia kwa Wahasibu Afrika




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza wakati akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ufungaji wa Mkutano wa Pili wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Nchi za Afrika (AAAG) uliofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC).

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko amewaasa wahasibu barani Afrika kuisimamia taaluma yao kikamilifu ili kuendeleza umuhimu na mchango na ukuaji wa uchumi duniani.

Ameyasema hayo Desemba 04, 2024 wakati akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ufungaji wa Mkutano wa Pili wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Nchi za Afrika (AAAG) uliofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC).

"Nataka niwaombe wahasibu mtambue kuwa taaluma yenu ni muhimu hata chochote kinachotokea katika sehemu zenu za kazi mtalaumiwa, hivyo mzuie hasara zinazoweza kutokea," amesema Dkt. Biteko.

Amewaasa kusimamia taaluma yao kwa kuzingatia misingi ya kitaaluma hata kama uamuzi wao unaweza kuwa na gharama" Isimamieni taaluma yenu kwa wivu mkubwa na kusema ukweli hata kama mtachukiwa, mahali pa kazi ili kuwe na ufanisi ni muhimu kuwaheshimu wahasibu ili wakupe matokeo tarajiwa,"

Aidha, Dkt. Biteko amesema ni muhimu kwa wahasibu hao kujiongezea ujuzi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

Pamoja na hayo amesema wahasibu wanatakiwa kuwa washauri wazuri wa viongozi wao ili waweze kufanya maamuzi sahihi, huku akisema AU inategemea wataalamu hao ili kuisaidia Afrika kunufaika na rasilimali zake.

"AU inawategemea nyie wimbo wa Afrika ni tajiri utabaki kwenye vitabu kama hatutachukua hatua," amesema Dkt. Biteko.

Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande amempongeza Mwenyekiti wa AAAG na Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Tanzania kwa kuandaa mkutano mzuri na kuwataka wahasibu kuzingatia maadili ya kazi yao.

"Afrika tuna utajiri wa kuwa na watu wenye uwezo mkubwa katika kada hii ya uhasibu na ni imani yangu kupitia mkutano huu utaleta mabadiliko katika nchi zetu," amesema Mhe. Chande.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Nchi za Afrika ambaye pia ni Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Lesotho, Malehlohonolo Mahase amesema kuwa Afrika inabadilika katika masula ya uhasibu na kupitia mkutano huo wamepata fursa ya kubadilishana mawazo na ujuzi.

Amesema AAAG ni bodi ya kiafrika inayolenga kwenda sambamba na Umoja wa Afrika huku ikisimamia nguzo za Umoja huo na kuwa mikataba inayoridhiwa na AU inatekelezwa pia na AAAG ili kuwa na ukuaji endelevu kwa nchi wanachama na Afrika kwa ujumla.

"Kipaumbele chetu kimekuwa ni wahasibu wanavyoweza kusimamia masula ya uhasibu ikiwemo hazina za nchi zetu, tumezungumzia kada ya uhasibu, kuimarisha mifumo yetu fedha na kushughulukia upotevu wa fedha katika nchi zetu," amesema Mahase.

Mahase amewataka Wahasibu Wakuu na Wahasibu Afrika kuendana na mabadiliko ya teknolojia katika taaluma yao sambamba na kujiongezea ujuzi ili kuwa na ufanisi katika kazi zao.

Ametaja umuhimu wa wataalamu hao na kusema kuwa Afrika inawahitaji zaidi wakati huu ili kukusanya mapato na kuzuia njia zisizo halali za mianya ya fedha.

Akizungumzia baadhi ya maazio ya mkutano huo "Mkutano huu umeazimia kuwa na matumizi bora ya rasilimali, kutumia mifumo ya kihasibu inayoshabihiana, kuwa mafunzo ya mara kwa mara kwa watu wa kada ya uhasibu,"

Amesisitiza "Kuongeza ushiriki wa wananchi kuhusu bajeti katika utekelezaji na utoaji taarifa ili kuongeza uwazi sambamba na kuwekeza kwenye masuala ya usalama mtandaoni,"


Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Nchi za Afrika, Fredrick Riaga ameipongeza Tanzania kwa kuhakikisha mkutano huo unafanyika kwa mafanikio makubwa.

Amewashukuru Wahasibu Wakuu kutoka nchi mbalimbali walioshiriki akisema ni kiashiria cha kuimarisha sekta ya uhasibu Afrika ambapo washiriki 800 wametoka Tanzania huku mkutano wote ukiwa na idadi ya washiriki 1,000 ambapo zaidi ya washiriki 1500 wamehudhuria mkutano huo kutoka nchi 26 barani Afrika.

Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Tanzania, Leonard Mkude amewasihi washiriki wa mkutano huo kufanyia kazi yote waliyojifunza ili kuboresha kazi za uhasibu katika nchi zao.

# SERIKALI YASEMA UNYANYASAJI DHIDI YA WENYE ULEMAVU SASA BASI

- Dkt. Biteko asema Serikali itakula Sahani moja na wanyanyasaji wa wenye ulemavu
- Wakuu wa Mikoa waagizwa kusimamia mpango wa taifa haki na Ustawi kwa wenye ulemavu
- Halmashauri zatakiwa kutenga Bajenti ununuzi wa teknolojia saidizi kwa wenye ulemavu




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza na wananchi mbalimbali waliojitokeza kushuhudia Mpango Kazi wa Taifa wa Haki na Ustawi wa watu wenye Ualbino na Mkakati wa Taifa wa Teknolojia kwa wenye Ulemavu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani iliyoadhimishwa katika Ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salam.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko amewaasa wahasibu barani Afrika kuisimamia taaluma yao kikamilifu ili kuendeleza umuhimu na mchango na ukuaji wa uchumi duniani.

Ameyasema hayo Desemba 04, 2024 wakati akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika ufungaji wa Mkutano wa Pili wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Nchi za Afrika (AAAG) uliofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC).

"Nataka niwaombe wahasibu mtambue kuwa taaluma yenu ni muhimu hata chochote kinachotokea katika sehemu zenu za kazi mtalaumiwa, hivyo mzuie hasara zinazoweza kutokea," amesema Dkt. Biteko.

Amewaasa kusimamia taaluma yao kwa kuzingatia misingi ya kitaaluma hata kama uamuzi wao unaweza kuwa na gharama" Isimamieni taaluma yenu kwa wivu mkubwa na kusema ukweli hata kama mtachukiwa, mahali pa kazi ili kuwe na ufanisi ni muhimu kuwaheshimu wahasibu ili wakupe matokeo tarajiwa,"

Aidha, Dkt. Biteko amesema ni muhimu kwa wahasibu hao kujiongezea ujuzi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

Pamoja na hayo amesema wahasibu wanatakiwa kuwa washauri wazuri wa viongozi wao ili waweze kufanya maamuzi sahihi, huku akisema AU inategemea wataalamu hao ili kuisaidia Afrika kunufaika na rasilimali zake.

"AU inawategemea nyie wimbo wa Afrika ni tajiri utabaki kwenye vitabu kama hatutachukua hatua," amesema Dkt. Biteko.

Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande amempongeza Mwenyekiti wa AAAG na Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Tanzania kwa kuandaa mkutano mzuri na kuwataka wahasibu kuzingatia maadili ya kazi yao.

"Afrika tuna utajiri wa kuwa



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizindua Mpango Kazi wa Taifa wa Haki na Ustawi wa watu wenye Ualbino na Mkakati wa Taifa wa Teknolojia kwa wenye Ulemavu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani iliyoadhimishwa katika Ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salam.



Watoto wenye ulemavu kutoka Shule ya Salvation Army, Kurasini Jijini Dar es Salaam wakipokea Mkono wa Pongezi wa Mgeni rasmi, Dkt. Doto Biteko baada ya kutumbuiza katika Maadhimisho ya Siku ya Walemavu Duniani yaliyofanyoka Diamond Jubilee, Jijini Dar es Salaam.

na watu wenye uwezo mkubwa katika kada hii ya uhasibu na ni imani yangu kupitia mkutano huu utaleta mabadiliko katika nchi zetu," amesema Mhe. Chande.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Nchi za Afrika ambaye pia ni Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Lesotho, Malehlohonolo Mahase amesema kuwa Afrika inabadilika katika masula ya uhasibu na kupitia mkutano huo wamepata fursa ya kubadilishana mawazo na ujuzi.

Amesema AAAG ni bodi ya kiafrika inayolenga kwenda sambamba na Umoja wa Afrika huku ikisimamia nguzo za Umoja huo na kuwa mikataba inayoridhiwa na AU inatekelezwa pia na AAAG ili kuwa na ukuaji endelevu kwa nchi wanachama na Afrika kwa ujumla.

"Kipaumbele chetu kimekuwa ni wahasibu wanavyoweza kusimamia masula ya uhasibu ikiwemo hazina za nchi zetu, tumezungumzia kada ya uhasibu, kuimarisha mifumo yetu fedha na kushughulukia upotevu wa fedha katika nchi zetu," amesema Mahase.

Mahase amewataka Wahasibu Wakuu na Wahasibu Afrika kuendana na mabadiliko ya teknolojia katika taaluma yao sambamba na kujiongezea ujuzi ili kuwa na ufanisi katika kazi zao.

Ametaja umuhimu wa wataalamu hao na kusema kuwa Afrika inawahitaji zaidi wakati huu ili kukusanya mapato na kuzuia njia zisizo halali za mianya ya fedha.

Akizungumzia baadhi ya maazio ya mkutano huo "Mkutano huu umeazimia kuwa na matumizi bora ya rasilimali, kutumia mifumo ya kihasibu inayoshabihiana, kuwa mafunzo ya mara kwa mara kwa watu wa kada ya uhasibu,"

Amesisitiza "Kuongeza ushiriki wa wananchi kuhusu bajeti katika utekelezaji na utoaji taarifa ili kuongeza uwazi sambamba na kuwekeza kwenye masuala ya usalama mtandaoni,"


Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Wahasibu Wakuu wa Nchi za Afrika, Fredrick Riaga ameipongeza Tanzania kwa kuhakikisha mkutano huo unafanyika kwa mafanikio makubwa.

Amewashukuru Wahasibu Wakuu kutoka nchi mbalimbali walioshiriki akisema ni kiashiria cha kuimarisha sekta ya uhasibu Afrika ambapo washiriki 800 wametoka Tanzania huku mkutano wote ukiwa na idadi ya washiriki 1,000 ambapo zaidi ya washiriki 1500 wamehudhuria mkutano huo kutoka nchi 26 barani Afrika.

Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Tanzania, Leonard Mkude amewasihi washiriki wa mkutano huo kufanyia kazi yote waliyojifunza ili kuboresha kazi za uhasibu katika nchi zao.

# MAGU WAMSHUKURU RAIS SAMIA, DKT. BITEKO AWAHAKIKISHIA MAENDELEO

- 99% YA VIJIJI VYAFIKISHIWA UMEME MAGU
- MAJIKO YA GESI 3,255 KUSAMBAZWA KWA BEI YA RUZUKU MAGU



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza na wananchi katika Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Jimbo la Magu uliofanyika Desemba 23, 2024 katika Kijiji cha Ijinga kilichopo Wilayani Magu Mkoani Mwanza.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewahakikishia wananchi wa Kijiji cha Ijinga kilichopo kwenye Kisiwa Wilayani Magu Mkoani Mwanza kijiji pekee kilichosalia kufikishiwa umeme wilayani humo kitafikiwa na kwamba zaidi ya shilingi milioni 600 imetengwa na Mkandarasi yupo eneo la mradi.

Amesema hayo Wilayani Magu Desemba 23,2024 wakati akihutubia wananchi katika Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Jimbo la Magu.

"Mnavijiji 82, vijiji 81 vyote vina umeme kimebaki kijiji kimoja kipo kwenye kisiwa na tuliona itachukua muda kuwapelekea umeme kwa kulaza nyaya kwenye maji tukaona watu wa Ijinga ni Watanzania wanastahili kupata umeme tumetenga milioni 619 ili nao wapate umeme," alisema

Mhe. Biteko Alisema Mkandarasi yupo eneo la mradi Kampuni ya Master Volt Ltd yupo kwa ajili ya kupeleka umeme Jua (Solar).

Kwa upande wake Mbunge wa Magu, Mhe. Boniventura Kiswaga alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kufikisha umeme katika vijiji 81 kati ya vijiji 82 jimboni humo.

"Kazi kubwa imefanyika, umeme sasa 99%, tumebakiza kijiji kimoja tu cha Ijinga kwani vijiji 81 tayari vyote vina umeme," alisema.

Aidha alimshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuibeba ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia ambayo alisema inakwenda kuokoa mazingira na afya zao.

"Naipongeza REA kwa kuibeba ajenda hii ya Mhe. Rais kwa kuandaa programu mbalimbali ikiwemo ya usambazaji wa majiko ya gesi kwa bei ya ruzuku ya 50%," alisema Mhe. Kiswaga.




Wananchi wakipata elimu kuhusu majiko banifu pamoja na majiko ya umeme wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Jimbo la Magu uliofanyika Desemba 23, 2024 katika Kijiji cha Ijinga kilichopo Wilayani Magu Mkoani Mwanza.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini, Msimamizi wa Miradi Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Awesa Rashid alisema REA inatekeleza miradi mbalimbali mkoani humo na kwamba baada ya kukamilisha kusambaza umeme vijijini na sasa ni zamu ya vitongoji.

"Tunatekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji 15 kwa kila Jimbo ikiwemo Jimbo la Magu ambapo kwa sasa mradi huu unaendelea," alifafanua Mhandisi Awesa.

Alitoa wito kwa wananchi kuchangamkia fursa ya kuunganishiwa umeme kwa bei ya shilingi 27,000 tu ili kujiletea maendeleo.

Aidha, akizungumzia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia 2024-2034, Mhandisi wa Miradi kutoka REA, Ramadhani Mganga alisema REA inaendelea kuhamasisha wananchi kutumia bidhaa za nishati safi za kupikia ili kuepukana na adha mbalimbali zinazotokana na matumizi ya nishati zisizo safi.

"Tumuunge mkono Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ili kuhakikisha 80% ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ifikapo mwaka 2034," alisema Mhandisi Mganga.

Mhandisi Mganga alisema kwa upande wa Mkoa wa Mwanza jumla ya majiko 19,530 yatasambazwa ambapo kila wilaya itapata majiko 3,255 kwa bei ya ruzuku ya asilimia 50%.

"Tupo hapa kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi. Napenda kuwahimiza wananchi wanapokwenda kununua mtungi huu wa ruzuku ni lazima uwe na kitambulisho cha Taifa," alisisitiza.

Kwa nyakati tofauti wananchi waliipongeza Serikali kupitia REA kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika suala zima la matumizi ya nishati safi.

"Mpango huu wa Serikali tumeupokea vizuri. Tunamshukuru Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani ameturahisishia sisi watanzania tulikuwa tunakata miti ovyo ili kupata kuni na mkaa na sasa madhara yake tunayaona," alisema Sebastian Boniphace Mkazi wa Magu.

# WANANCHI WAMPONGEZA RAIS SAMIA UTEKELEZWAJI MIRADI YA UMEME VIJIJINI

- 99% YA VIJIJI VYAFIKISHIWA UMEME MAGU
- MAJIKO YA GESI 3,255 KUSAMBAZWA KWA BEI YA RUZUKU MAGU



Wajumbe wa Bodi ya Nishati Vijijini (REB) wakiwa wameongozana na Menejimenti ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wakikagua miundombinu ya umeme katika Kijiji cha Keichuru kilichopo katika Wilaya ya Kibiti Mkoa wa Pwani wakati wa ziara ya Bodi hiyo kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Wakala nchini.

Wananchi wa Kijiji cha Keichuru kilichopo katika Wilaya ya Kibiti Mkoa wa Pwani wamempongeza na kumshukuru Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kwa utekelezwaji wa miradi ya kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Wananchi hao wametoa pongezi hizo leo wakati wa ziara ya Bodi ya Nishati Vijijini (REB) kutembelea na kukagua maendeleo ya mradi wa kupeleka umeme katika vijiji vivyopo katika Delta wilayani Kibiti.

“Kwanza tutoe shukrani kwa taasisi zote zilizowezesha umeme kufika hapa kijijini kwetu na pongezi na shukrani nyingi kwa mama yetu Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha zilizowezesha hata sisi kufikiwa na umeme. Hata wazazi wetu wangekuja wangeshangaa sana,” amesema Mzee Hassan Malinda.

Naye Mama Anna Hamis amesema kuwa hawakutegemea umeme utafika katika kijiji chao licha ya kuwa kipo katika eneo la Delta kikiwa kimezungukwa na maji.

Mzee Iddi Ali ameshuru kwa kijiji chao kufikishiwa umeme na kusema kuwa na wao sasa wanaona matunda ya uhuru na kuhamasisha vijana kutumia umeme huo kujiletea maendeleo.

Awali akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Mhe. Balozi Radhiya Msuya amesewahamashisha wananchi hao waanze kufunya maandalizi



Miundombinu ya umeme ikiwa imefika katika Kijiji cha Keichuru kilichopo katika Wilaya ya Kibiti Mkoa wa Pwani.

katika nyumba zao kwa kusambaza nyaya ndani ya nyumba ili umeme huo utakapowashwa waweze kuunga.

"Mhe. Rais anahaingaika usiku na mchana kutafuta fedha kwa ajili ya maendeleo yetu. Na namna pekee ya kumshukuru kwa kile anachofanya ni kuunganisha nyumba zetu na umeme huu pamoja na kutumia umeme huu kwa shughuli za maendeleo na kukuza uchumi wetu wa mtu mmoja mmoja na jamii zetu kwa ujumla," amesema Balozi Msuya.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Saidy amewataka wananchi hao kutunza na kuwa walinzi wa miundombinu ya umeme kama nyaya, nguzo na mashine umba (transfoma) kwa sababu serikali imetumia gharama kubwa kufikisha miundombinu hiyo.


"Zaidi ya Shilingi Bilioni 3.8 zimetumika kufika umeme katika vijiji hivi vilivyopo katika Delta katika Wilaya hii. Ni muhimu sana sisi tukawa walinzi wa miundombinu hii," amesisitiza Mhandisi Saidy.

Mbunge wa Jimbo la Kibiti, Mhe. Twaha Mpembenwe amemshukuru Mhe. Rais kwa miradi mbalimbali ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa katika Jimbo lake hasa miradi ya umeme vijijini na kuahidi kuwa yeye pamoja na wananchi katika jimbo hilo watakuwa walinzi wa kwanza wa miundombinu ya umeme ikiwa ni njia ya kuendelea kuthamini mchango wa Serikali katika kuwaletea maendeleo.

Augustino Kiwia ambaye ni Mwakilishi wa Mkandarasi anayetekeleza mradi huo ambao ni Kampuni ya CRCEBG, amesema kuwa changamoto kubwa inayowakabili ni kukatika kwa daraja na hivyo kushindwa kusafirisha nguzo za zege kwa njia ya mitumbwi. Ameahidi kuwa, pindi daraja hilo litakapokuwa limejengwa wataharakisha kazi hiyo ikamilike kwa wakati.

# REA KUSAMBAZA MITUNGI YA GESI 13,020 KWA BEI YA RUZUKU MKOANI SHINYANGA

- 99% YA VIJIJI VYAFIKISHIWA UMEME MAGU
- MAJIKO YA GESI 3,255 KUSAMBAZWA KWA BEI YA RUZUKU MAGU



Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Bi Martha Chassama (kulia) pamoja na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga Mhe Santiel Kirumba (wa pili kulia) wakimpa mmoja wa wananchi wa mkoani Shinyanga mtungi wa gesi ikiwa ni ishara ya kuzindua kampeni ya ugawaji wa mitungi ya gesi kwa bei ya ruzuku katika Mkoa huo kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia. Kushoto ni Mhandisi kutoka REA, Mhandisi Ramadhani Mganga.

Wakala wa Nishati Vijijini (REA) unaendelea kutekeleza Mradi wa usambazaji wa mitungi ya gesi ya kilo 6 kwa bei ya ruzuku, ambapo inatarajia kugawa mitungi 13,020 katika mkoa wa Shinyanga, Mradi huo utagharimu jumla ya shilingi milioni 545.538

REA, iliingia mkataba na mtoa huduma; kampuni ya Lake Gesi, kampuni ambayo, itahudumia wilaya 4 za Mkoa wa Shinyanga kwa kuuza mitungi hiyo ya gesi ya kilo 6 kwa bei ya ruzuku ya shilingi 20,950 pamoja na vifaa vyake, katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji.

Hayo yameelezwa na Mhandisi Miradi wa Wakala wa Nishati Vijijini-REA Mhandisi Ramadhani Mganga tarehe 19 Disemba 2024 wakati akizungumza na Wakunga, Wauguzi, kina mama waliojifungua watoto njiti na Mama wajawazito katika Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu Wilayani Kahama na kuwagawia mitungi ya gesi ya Kilo sita kila mmoja ambapo jumla ya mitungi 100 imetolewa yenye thamani ya shilingi Milioni 4.1

Akizungumza kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa REA Bi Martha Chassama amesema kuwa kazi ya Serikali ni kuhakikisha nishati safi za kupikia zinawafikia Wananchi wa vijijini kwa ukaribu zaidi na kwa bei nafuu na kuongeza kuwa Serikali inafanya kwa kushirikiana na Sekta Binafsi.



Mwakilishi wa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Bi Martha Chassama (wa pili kulia) pamoja na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga Mhe Santiel Kirumba (katikati) wakiwa kwenye picha ya pamoja na wananchi wa mkoani Shinyanga waliopata mitungi ya gesi ikiwa ni ishara ya kuzinduliwa kwa kampeni ya ugawaji wa mitungi ya gesi kwa bei ya ruzuku katika Mkoa huo kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia. Kushoto ni Mhandisi kutoka REA, Mhandisi Ramadhani Mganga.

Chassama amesisitiza umuhimu wa matumizi sahihi ya gesi hizo walizopewa huku akieleza kuwa wilaya zitakazofikiwa na mradi huo katika mkoa wa Shinyanga ni pamoja na Kishapu, Shinyanga na Halmashauri ya Ushetu na Msalala.

Mbunge wa Vitimaalum Mkoa wa Shinyanga Mhe Santiel Kirumba ameupokea mradi huo ambapo amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mstari wa mbele na kuipa REA fedha kwa ajili ya kuhakikisha wanawake wanatumia nishati safi na salama ambayo pia itaokoa muda na afya za watumiaji ikiwemo kuokoa mazingira.

“Nishati salama ni mtaji wa afya zetu, ni mkombozi wa uchumi, Inaepusha wanawake na ukatili wa kijinsia, hivyo nampongeza sana Mhe Rais Dkt Samia kupitia taasisi ya REA kwa kumjali mwanamke na watanzania kwa ujumla wake” Amekaririwa Mhe Kirumba

For more info
**www.nishati.go.tz**

